

# AFYA NJEMA, SINA MADINI YA RISASI!




Copyright 2021 NH DHHS

Imeandikwa na Gail C. Gettens na Knatalie Vetter

Imechorwa na Allison Valentine

Familia yetu inaanza kuongezeka,  
tunamtarajia mtoto mwingine.  
Tunahitaji nafasi zaidi  
ili kukua na kucheza.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Madini ya risasi ni sumu inayodhuru takribani kila sehemu ya mwili wa mtoto haswa ubongo.

Hatua rahisi zinaweza kusaidia kumlinda mtoto wako kutopata madini ya risasi.



Copyright 2021 NH DHHS



Copyright 2021 NH DHHS

Unatafuta mahali kubwa,  
tunajifunza tukiwa popote.  
Tungependa kujua ikiwa kuna  
rangi ya madini ya risasi.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Kabla ya kununua ama kupangisha nyumba iliyojengwa kabla ya 1978, kisheria, unapaswa kupokea kijitabu cha *Protect Your Family from Lead in Your Home* (Ilinde Familia Yako dhidi ya Madini ya Risasi Nyumbani Kwako).

Nyumba zilizojengwa kabla ya 1978 zinaweza kuwa na rangi na vumbi lililo na madini ya risasi.

Kabla ya kupasha joto na kuongeza  
mwangaza kwenye vyumba,  
tunaangalia maadini ya  
risasi ili kukarabati vizuri.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Kabla hujaamua kununua au kukarabati nyumba, mkaguzi wa madini ya risasi aliye na leseni anaweza kupima kwa rangi iliyo na madini ya risasi.

Ukaguzi wa nyumba haujumuishi kipimo cha rangi iliyo na madini ya risasi.




Copyright © 2021 NH DHHS



Copyright 2021 NH DHHS

Kwa kutumia kifaa cha kupima,  
ncha ya sponji inabadilika  
inageuka nyekundu.  
Sasa tunajua mahali  
madini ya risasi yalipo.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Kiasi cha vumbi lenye madini ya risasi kinachoweza kumsumu mtoto ni kidogo sana, huwezi kukiona kwenye mikono, midoli, sakafu wala sehemu nyingine za juu.

Unaweza kununua vifaa vya vipimo vya madini ya risasi vinavyotambuliwa na EPA kwenye duka la vifaa vya ujenzi.

Tunajitayarisha kwa safari yetu.  
Itakuwa raha!  
Kukaa mbali na  
nyumbani hadi kazi ikamilike.



Wazazi, mlijua kwamba:

Watoto na kina mama wajawazito wanapaswa kuondoka hadi kazi isiyoleta madini ya risasi ikamilike na eneo lisafishwe kabisa.

Kazi inayovuruga rangi yenye madini ya risasi husababisha vumbi hatari lenye madini ya risasi.



Copyright 2021 NH DHHS



Copyright 2021 NH DHHS

Kufanya kazi salama isiyo  
na madini ya risasi  
ni muhimu ili kulinda familia  
yetu na wafanyakazi pia.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Wakarabati walioidhinishwa katika desturi za kazi zisizo na madini ya risasi pia wanafunzwa ili kuangalia madini ya risasi na kutoa kijitabu cha *Haki ya Ukarabati*.

Mafunzo ya ukarabati wa mazingira yasiyo na madini ya risasi kinapatikana kwa wamiliki wa nyumba.

Familia yetu inakusanyika  
pamoja kuuzima mshumaa.  
Inaimba “Happy Birthday”  
ili kusherehekea mwaka mmoja.



Wazazi, mlijua kwamba:

Watoto wanaoonekana na furaha na wenye afya bora wanaweza kuwa na viwango hatari vya madini ya risasi kwenye mili yao.

Viwango vya madini kwa watoto vinapaswa kupimwa wakiwa na umri wa mwaka 1 na pia miaka 2.



Copyright 2021 NH DHHS





Unapoenda kumwona daktari katika umri wa mwaka mmoja na miaka miwili, kipimo cha kiwango cha madini ya risasi ndicho tutakachofanya.



Wazazi, mlijua kwamba:

Kiwango cha madini ya risasi cha mtoto wako kinaweza kupimwa katika ofisi ya daktari kwa kutoboa tundu dogo kwenye kidole.

Matokeo ya vipimo yanapatikana kabla hujaondoka kwenye ofisi.

Tunamchunguza mtoto kutoka kichwani hadi kwenye vidole vya miguu, kipimo cha haraka cha kiwango cha madini ya risasi kabla hatujaenda.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Kumnavya mtoto wako mikono kwa sabuni na maji ni muhimu kabla ya kula, kulala na kupima kiwango cha madini ya risasi ili kuondoa chembechembe za madini ya risasi.

Pamba za alkoholi na sanitaiza za mikono haziondoi madini ya risasi.



Copyright 2021 NH DHHS



Kucheka pamoja na  
kucheza na midoli,  
nyumba yetu imejaa  
kelele za furaha.



**Wazazi, mlijua kwamba:**

Kuna maeneo mengi nyumbani na katika mazingira yako ambayo madini ya risasi yanaweza kupatikana, ikiwemo rangi, vumbi, mchanga, midoli na maji.

Madini ya risasi yanaweza kupelekwa nyumbani kutoka kwenye aina fulani za kazi na mambo yanayokuvutia.

Kuchukua hatua rahisi kunaweza kutufanya kuwa na afya njema, kutokuwa na madini ya risasi!



Wazazi, mlijua kwamba:

Hakuna kiwango salama cha hatari ya madini ya risasi kwa watoto; hata viwango vidogo ni vibaya kwa afya, maendeleo ya ubongo na ukuaji wao.

Sumu ya madini ya risasi inaweza kuzuiwa kwa asilimia 100.



Copyright 2021 NH DHHS

# Ili kupata maelezo zaidi, tembelea [LeadFree.Me](https://www.leadfree.me)



## Usaidizi wa matibabu umetolewa na NH Chapter of the American Academy of Pediatrics.

Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya NH (NH DHHS) iliunda kitabu hiki kwa mikataba iliyoifadhiliwa na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani (HHS), Centers for Disease Control and Prevention (CDC) na U.S. Environmental Protection Agency (EPA). Yaliyomo ni yale ya NH DHHS na huenda yasiakisi sera rasmi au maoni, wala kuidhinishwa na HHS, CDC au EPA.

Maelezo yanayotolewa katika kijitabu hiki yanatokana na uelewa wa sasa wa sayansi na ufundi wa masuala yaliyowasilishwa. Kufuata ushauri uliotolewa hakutataa ulinzi kamili katika hali zote wala dhidi ya hatari zote za afya zinazoweza kusababishwa na athari ya madini ya risasi.



PINT SIZE PRODUCTIONS, LLC  
Amherst, New York 14221 • Sanborn, New York 14132  
Conforms to ASTM and CPSIA testing requirements.  
Proudly manufactured in the USA.  
[PINTSIZEPRODUCTIONS.COM](http://PINTSIZEPRODUCTIONS.COM)



Distributed by  
**Cribs for Kids LLC.**  
TO ORDER BOOKS:

